



BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA SITA

Kikao cha Thelathini na Nne – Tarehe 23 Juni, 2017.

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

- I. **TAARIFA YA SPIKA:**
- II. **HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Ripoti ya Utekelezaji ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar Kuhusu Utekelezaji kwa kipindi cha Oktoba 2013 - Disemba 2016.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mahakama ya Kadhi Nam. 3 ya 1985 na Kuanzisha Upya Mahakama ya Kadhi na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Baraza la Taifa la Biashara na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum:

Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kuhusu Ripoti ya Utekelezaji ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar Kuhusu Utekelezaji kwa kipindi cha Oktoba 2013 - Disemba 2016.

III. MASWALI:

Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

154. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inajitahidi sana katika kuleta maendeleo ya Zanzibar na wananchi wake lakini katika kisiwa cha Pemba suala la Tanki la Mafuta bado ni changamoto kwani pamoja na kuwa na shida ya mafuta, lakini lipo tanki moja tu la kuweka mafuta.

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza matanki ya kuweka mafuta ya Petroli, Diesel na Mafuta ya taa.
- (b) Kama mpango upo ni lini suala hili litatekelezwa na kama halipo Serikali inalionaje suala hili.
- (c) Je, yapo maeneo yaliyotengwa kwa shughuli ya kuweka mafuta Pemba na kama hayapo, Serikali haioni umuhimu huo kabla Serikali haijaingia migogoro na wananchi kwa ajili ya maeneo.

IV. TAARIFA ZA SERIKALI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Ripoti ya Utekelezaji ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar Kuhusu Utekelezaji kwa kipindi cha Oktoba 2013 - Disemba 2016.

V. **HOJA ZA SERIKALI:**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mahakama ya Kadhi Nam. 3 ya 1985 na Kuanzisha Upya Mahakama ya Kadhi na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo – Kusomwa kwa Mara ya Kwanza.

Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Baraza la Taifa la Biashara na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo – Kusomwa kwa Mara ya Kwanza.

Zanzibar,
23 Juni, 2017.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.